# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA SABA

**06 NOVEMBA, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

_______________________

# MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA SABA – TAREHE 06 NOVEMBA, 2024

## I. DUA:

## II. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**107. MHESHIMIWA HASAN SELEMANI MTENGA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, kwa nini Meneja Rasilimali Watu wa kiwanda cha Simenti cha Dangote Mtwara ni Raia wa Nigeria wakati Sheria inamtaka awe Mtanzania.

**108. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali imeweka mazingira gani ya kuwavutia Wataalam Wabobezi kutoka nje na wangapi ni Watanzania na wangapi wanafanya kazi nje.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**109. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini mkakati wa Serikali wa kumaliza upungufu mkubwa wa Walimu kwa shule za Msingi nchini.

**110. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Barabara za Juhudi, Dumbalume, Kwayamba, Kwamnyani/Kwa Nyoka, Sekondari, Bakhresa/Kingugi na Kibudi/Moringe zitajengwa.

**111. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Pagwi - Kilindi.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**112. MHESHIMIWA ABDUL YUSSUF MAALIM (AMANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wigo wa biashara ya Hewa Ukaa ili kupunguza ukataji wa Misitu nchini.

**WIZARA YA NISHATI:**

**113. MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itapeleka Mradi wa REA kwenye Mitaa ya Tampori, Kwamtwara, Chemichemi, Chandimo, Dumi, Hachwi na Guruma - Kondoa.

**114. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza baadhi ya kodi ili Watanzania wengi waweze kuingiza magari yenye mfumo wa Nishati ya Gesi.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**115. MHESHIMIWA MARY FRANCIS MASANJA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali inawasaidiaje waathirika wa matendo ya unyanyasaji wa kijinsia baada ya hatua za kisheria kuchukuliwa.

**WIZARA YA UJENZI:**

**116. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Choma - Ziba - Nkinga hadi Puge utaanza.

**117. MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini matuta na vivuko vya waenda kwa miguu vitawekwa katika Barabara ya Lupaso - Lwangwa - Mbambo hadi Tukuyu.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**118. MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU (KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ipi kauli ya Serikali kuhusu uzalishaji wa bidhaa zenye viwango hafifu na ukubwa tofauti zikiwa na bei sawa sokoni.

**WIZARA YA MAJI:**

**119. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji uliokwama kwa muda mrefu katika Kijiji cha Mang'ola juu Wilayani Karatu.

## WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

**120. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itapeleka minara ya simu eneo la Nyamohonda na Itiryo - Tarime Vijijini.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**121. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Meli moja ya Uvuvi Ziwa Nyasa ili Samaki wakubwa wanaoishi kwenye kina kirefu wasiendelee kufa.

**122. MHESHIMIWA DKT. ANGELINE SYLVESTER LUBALA MABULA (ILEMELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani kukopesha vifaa vya kukaushia Samaki na Dagaa pale ambapo Mwananchi anahitaji kukopa.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**123. MHESHIMIWA AMINA ALI MZEE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itaanza kuweka Sheria na Utaratibu mzuri wa kupunguza ajali za Barabarani zitokanazo na uzembe wa Madereva.

**III. KAMATI YA MIPANGO:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **06 NOVEMBA, 2024** | **KATIBU WA BUNGE** |

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA